# Ulega aagiza mbegu mpya za malisho zisambazwe vijijini

## ■ Lengo ni kukomesha migogoro ya wafugaji na wakulima

**Kibaha**
**NA SCOLASTICA MSEWA**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amemwagiza Katibu Mkuu anayeshugulikia Mifugo Profesa Elisante Ole Gabriel, kuhakikisha aina mpya ya malisho kutoka China yanayojulikana kama Juncao, mbegu zinasambazwa kote hadi kwa wafugaji vijijini.

Alisema hayo alipotembelea na kukagua maendeleo ya Shamba la Malisho ya Mifugo lilipo Vikuge wilayani Kibaha mkoani Pwani.

Ulega alisema mbegu za majani hayo zisambazwe kuanzia ngazi ya mikoa, wilaya hadi vijiji lengo likiwa kudhibiti mifugo na wafugaji kuhamahama kutafuta malisho.

Alisema hataki kuona mambo yanayoanzishwa kwa ajili ya kunufaisha wananchi yanaishia njiani kwani ni vizuri kukawa na mwendelezo wa teknolojia hiyo ya kilimo hicho kipya cha malisho ya mifugo hata kusambazwa kwa wafugaji hadi vijijini.

Ulega alisema walengwa wa zao hilo jipya la juncao la malisho kwa mifugo ni wafugaji wa vijijini huku lengo la serikali ni kueneza hadi vijijini kwa wafugaji.

Alisema Juncao inatakiwa ienee hadi kwenye maeneo yenye ukame ya mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara, Shinyanga na iwapo itasambazwa vizuri itapunguza tatizo la wafugaji na mifugo yao kuhama hama kutafuta malisho ya mifugo yao.

"Kinachosababisha wafugaji kuzunguka na kuhama hama ni kutafuta chakula cha malisho na maji kwa ajili ya mifugo, hivyo kama wafugaji watafikishiwa mahali walipo itasaidia wafugaji." alisema Ulega.

"Iwapo malisho ya uhakika na maji yatasamba nchini kote hadi vijijini, wafugaji na mifugo yao hawatahama hama na kusababisha ugomvi usiokuwa na sababu, kwa hiyo nataka kuona inawafikia walengwa," alisema Naibu Waziri Ulega.

Aliongeza kuwa mbegu hizo zinapaswa zifike kwa haraka na kwa gharama nafuu ambayo kila mfugaji ataweza kumudu kununua ili aweze kuhudumia mifugo yake.

Naibu waziori huyo alisema wizara inapaswa ishirikiane na uongozi wa mikoa, wilaya na halmashauri ili kuhakikisha mbegu hizo zinafika kwa walengwa, kwa haraka na gharama nafuu.



MKURUGENZI Msaidizi Rasilimali za Vyakula vya Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Rogers Shengoto (wa tatu kulia) akionyesha aina mpya ya mbegu za majani ya chakula cha mifugo ya JUNCAO kwa Naibu Waziri wa Mifugo, Abdallah Ulega (katikati) wakati alipotembelea shamba la Vikuge mkoani Pwani juzi. Wa pili kushoto ni Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete. (Picha na Scolastica Msewa)

Akizungumzia changamoto wanazokutana nazo katika uendeshaji wa shamba hilo la Vikuge, Meneja Reuben Ngailo, alisema eneo hilo lina visiki vingi na ili kuving'oa inagharimu kiasi kikubwa cha fedha jambo ambalo husababisha kuendesha uzalishaji wa malisho katika eneo dogo.

Mbunge wa Chalinze, Ridhiwan Kikwete, akiwa ameambatana na naibu waziri aliomba malisho yanayozalishwa shambani hapo yawanufaishe watu wote wa Mkoa wa Pwani.

Ridhiwani alisema shamba hilo liko Pwani na mkoa huo una migogoro mingi ya wakulima na wafugaji kwa ajili ya kutafuta malisho na maji, hivyo ombi lake ni mbegu hizo zisambazwe haraka kwa wafugaji wa mkoa huo kwanza.

Akizungumza na uongozi wa Ranchi ya Mkata na wa Wilaya ya Kilosa, kuhusu namna bora ya kufanya ufugaji wa kibiashira, Ulega alisema serikali imechagua ranchi hiyo kuwa kituo cha kuzalisha mbuzi kwa wingi ambao watakuwa wanasambazwa katika maeneo mbalimbali nchini.

"Lengo ni kuwapelekea vikundi mbegu ya mbuzi ili waeneze na kila tutakayempa tutataka tujue yuko wapi na ana mbuzi wangapi ili tuwatambue na tuwaingize katika mfumo wetu wa takwimu za kibiashara ili iwapo tunapata mteja wa kilo 50 kwa mwezi kweli tuwe na uhakika wa kupata kilo hizo 50 kwa mwezi,"alisema Ulega.

Alisema kutokana na mkakati huo wa kopa mbuzi lipa mbuzi, mahitaji ya mbuzi yatakuja kuwa makubwa nchini, hivyo aliwataka kuzalisha mbuzi kwa wingi ili kuweza kutosheleza soko la ndani na nje ya nchi.

"Tuwe na takwimu kamili ili tukichukua mbuzi hapa na pale tunajua tutapata idadi inayotakiwa kwa hiyo nataka hapa Mkata pawe kituo cha kielelezo kwa mifugo ya mbuzi sio hawa ulionao 609...nikija tena baadaye mwaka huu nikute umeshaongeza idadi ya mbuzi," aliagiza Ulega.

"Najua sio rahisi sana, lakini jitahidi kuongeza idadi tutakupa ushirikiano wa kutosha ili kutimiza lengo la serikali tulilojiwekea."

"Washirikisheni wafugaji wabuni mbinu za kuongeza mbuzi na sasa hii ndio iwe biashara yenye wenyewe ni kuongeza idadi ya mbuzi ili lengo la kopa mbuzi lipa mbuzi litimie kwa kuuza mbuzi wengi nje ya nchi kama nchi za Uarabuni wanahitaji mbuzi wa Tanzania," alisema Ulega.

Aidha, Ulega alisema wafugaji hao wa mbuzi wafuge kibiashara ili kuweza kutimiza vigezo na masharti ya wateja wa kimataifa kama nchini hizo za Uarabuni ambazo wanataka mbuzi wenye uzito wa kilo kati ya nane hadi 10 ambao hawajakomaa sana.

Meneja wa Ranchi ya Mkata Kilosa, Oscar Magete, alisema ilianzishwa na serikali kwa madhumuni ya kuendeleza na kueneza ufugaji bora wa mbuzi, kondoo na ng'ombe ambapo ranchi hiyo ina ukubwa wa hekari 154,000 na kwa sasa ina mbuzi 609 kondoo 116 na ng'ombe 47.

Naye, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Hezron Nonga, akizungumzia masuala ya chanjo za mifugo alisema wameweza kutoa chanjo milioni 600 kwa mifugo nchini kutokana na chanjo zilizozalishwa nchini na nje ya nchi.

Alioongeza kuwa: "Tumeona kutoka mataifa mbalimbali

Scanned with CamScanner

# Wakazi 5,000 wapewa wafunzo ufugaji na kilimo

**Kahama**

**SALVATORY NTANDU**

ZAIDI ya wakulima na wafugaji 5,000 kutoka Kata ya Mwendakulima, Manipaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamenufaika katika uwekezaji wa sekta ya kilimo baada ya kuanzishwa kituo cha mafunzo ya kilimo na ufugaji kilichogharimu zaidi ya sh. milioni 500.

Akizungumza juzi baada ya uzinduzi wa kituo hicho, mkulima mkazi wa kata hiyo, Dewis Ntobi, alisema kabla ya kuanzishwa kwa kituo hicho alikuwa analima mahindi kiholela na kupata mazao kidogo.

Alisema baada ya kampuni ya uchimbaji wa madini ya Pangea inayomiliki mgodi wa Barrick Buzwagi kuanzisha kituo hicho ili kukabiliana na tatizo la ajira, wakulima na wafugaji wengi wa kata hiyo wamenufaika kwa kupata elimu ambayo imesaidia kulima na kufuga kwa utaalamu zaidi.

"Katika shamba langu nilikuwa napata gunia tano za mahindi kwa ekari mmoja ila baada ya kupata mafunzo haya kwa mwaka huu nimepata gunia 15, ambazo zitasaidia kujikwamua kiuchumi, nawaomba vijana wenzangu wajitokeze kuchangamkia fursa hii adhimu tuliyoipata,"alisema Ntobi.

Naye, mfugaji wa ngo'ombe wa maziwa, Zanura Masunga, alisema kuwa kituo hicho kimemsaidia kupata mbegu bora ya ng'ombe wa maziwa na nyama.

Alieleza kuwa wataalamu wa mifugo katika kituo hicho wamemsaidia kufanya uhamilishaji wa mbegu bora za ng'ombe chotara ambazo zinapatikana katika kituo hicho.

Mratibu wa mradi huo kutoka kampuni ya Barrick Buzwagi, Elibarick Jambau, alisema kituo hicho kimegharimu sh. milioni 529 ambapo kitasaidia wakulima na wafugaji kutapa elimu kwa njia za kisasa.

"Mpaka sasa zaidi ya wakulima 3,924 wameshapatiwa mafunzo ambapo awali walikuwa wanazalisha gunia 15 kwa ekari mmoja, lakini kwa msimu wa mwaka huu wameweza kuvuna gunia 28 kwa ekari mmoja, hatua hii itawasaidia kujikwamua kiuchumi,"alisema Jambau.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliwataka wakazi wa Kata ya Mwendakulima ambao wanauzunguka mgodi wa Buzwagi kuchangamkia fursa hiyo hususan vijana ili kujikwamua kiuchumi kwa sababu mafunzo yanayotolewa katika kituo hicho ni bure.

"Vijana jiungeni katika vikundi vya kilimo mfundishwe mbinu bora za kufanya kilimo au ufugaji wa kisasa katika maeneo yetu kupitia uwekezaji huu, Barrick wamejipanga kuwasaidia ili muondokane katika wimbi la umasikini," alisema.

*Alifafanua kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan* inalenga kuwawezesha wananchi kutumia fursa mbalimbali zilizopo katika maeneo yao kujipatia kipato.

Uhuru Uk.16, Julai 16,2021

Scanned with CamScanner

# Azaki zatakiwa kuelimisha vijana kilimo na ufugaji

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

Nipashe Uk.15, Julai 16,2021

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amelishauri Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kuwa daraja la kusaidia vijana kuwaelimisha kujitambua na kuchangamkia fursa za kilimo na ufugaji.

Pinda aliyasema hayo alipotembelewa na wajumbe wa baraza hilo nyumbani kwake Zuzu kwa lengo la kujifunza namna alivyowekeza katika sekta ya kilimo na ufugaji.

Alisema vijana wana nafasi kubwa kutoa mchango wa taifa, hivyo wanatakiwa kuchangamikia fursa zinazowazunguka hususan sekta ya kilimo na kubainisha kuwa kuna haja ya kuwa na kituo cha kilimo kila kanda, hali itakayochochea zaidi vijana kujikita kwenye sekta hiyo.

"Kwa takwimu zilizopo, kundi la hawa vijana ni kubwa sana, kikubwa ambacho mnatakiwa kukiangalia ni kuwaangalia hawa vijana kwa mawanda mapana kundi la vijana ambao hawakusoma na vijana wasomi, ukitaka kuwasaidia vijana lazima uangalie unafanyaje," alisema na kuongeza:

"Ushauri wa kwanza tujaribu kuwaasa vijana wajitambue kuwa wao sio taifa la kesho bali ni taifa la leo, yote na yote kama kijana lazima uangalie fursa zinazokuzunguka hivyo ninyi Baraza mnatakiwa muwe daraja la kuwaelimisha vijana wachangamkie fursa hasa kilimo."

Aidha, Pinda aliwaasa kuwa mstari wa mbele katika kuelimisha jamii kuondokana na hali ya utapiamlo nchini pamoja na mapambano dhidi ya umaskini.

Alitoa wito kuwa na uwazi masuala ya kifedha kwa asasi za kiraia ili kuaminika zaidi kwa serikali.

Naye Mwenyekiti wa Baraza hilo, Lilian Badi, alisema hatua ya ziara hiyo wamejifunza mengi kuhusu masuala ya kilimo huku akitoa ombi la kuwezeshwa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya baraza hilo.

Scanned with CamScanner

# Waziri: Shamba la mifugo liendeshwe kibiashara

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameagiza uongozi unaosimamia shamba la malisho ya mifugo lililopo Vikuge Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, kujiendesha kibiashara.

Pia ameuagiza kusambaza aina mpya ya mbegu za malisho ijulikanayo kama JUNCAO maeneo mbalimbali nchini kwa kuwa ina sifa ya kustahimili sehemu yenye ukame ili wafugaji wapande malisho hayo.

Ulega alisema hayo alipotembelea na kukagua maendeleo ya shamba hilo na kumwagiza Katibu Mkuu anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, kuhakikisha aina mpya hiyo ya malisho inasambazwa na kusimamiwa vyema ili ilete tija kwa taifa hususani kwa wafugaji vijijini.

Ulega aliagiza mbegu hiyo ya malisho ya JUNCAO isambazwe kuanzia ngazi ya mikoa, wilaya hadi vijijini, lengo likiwa ni kudhibiti mifugo na wafugaji kuhamahama kutafuta malisho.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha mbegu za malisho hayo zinaenea hadi vijijini kwa wafugaji hususani mikoa yenye ukame kama Dodoma, Singida, Manyara na Shinyanga.

"Kinachosababisha wafugaji kuzunguka na kuhama ni kutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao, hivyo kama watapata mbegu hiyo ya malisho na kuipanda mahali walipo itawasaidia kuwa na uhakika wa malisho hayo na kuacha kuhama hama," alisema Ulega.

Meneja wa shamba hilo la Vikuge, Reuben Ngailo, alisema changamoto wanazokutana nazo katika uendeshaji wa shamba hilo ni kukosekana kwa vifaa na nguvu kazi katika kusafisha shamba na kupanua uzalishaji.

Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, aliomba malisho yanayozalishwa shambani hapo kuhakikisha yanawanufaisha pia wakazi wa mkoa wa Pwani.

"Shamba hili lipo kwenye mkoa wa Pwani na ambao una migogoro mingi ya wakulima na wafugaji inayosababishwa na utafutaji wa malisho na maji, hivyo ombi langu ni mbegu hizi zisambazwe haraka kwa wafugaji wa mkoa huu ili itusaidie hata kupunguza migogoro ambayo imekuwa ikitokea baina ya pande hizi mbili za wakulima na wafugaji," alisema Ridhiwani.

Scanned with CamScanner

# Spread Juncao grass countrywide: Minister

By HILDA MHAGAMA

TO ensure the availability of livestock forage in the dry season, the government has directed the Vikuge Pasture seed farm at Kibaha–Coast region to spread Juncao grass technology in various parts of the country.

The Deputy Minister for Livestock and Fisheries, Mr Abdallah Ulega said Juncao is a hybrid grass and an important multi-functional agricultural resource and can also be used for mushroom farming or livestock forage and poultry feed.

**Mr Ulega made the remarks yesterday while concluding his two-day working visit to the region saying if the technology is distributed to the different districts and villages will control livestock and pastoralists migrating in pursuit of grazing.**

"This technology from China can bring tremendous changes to livestock keepers and the nation at large as its leaves, stems and roots are used for different ecological management, such as soil erosion control and desertification prevention," he said

Mr Ulega made the remarks yesterday while concluding his two-day working visit to the region saying if the technology is distributed to the different districts and villages will control livestock and pastoralists migrating in pursuit of grazing.

He said it was necessary to prioritise arid regions such as Dodoma, Singida, Manyara, and Shinyanga. The grass is likewise suitable for mushroom production.

Juncao, which means mushroom and grass, refers to a Chinese-invented technology using grass to grow mushrooms. Its use can help increase local income through low-cost mushroom cultivation and contain desertification by providing an added source of cattle feed.

The technology was invented by Professor Lin Zhanxi from China's Fujian Agriculture and Forestry University in the 1980s and has been shared with over 100 countries, including Tanzania.

"Juncao technology supports the 2030 Agenda for Sustainable Development, making an important contribution to several Sustainable Development Goals (SDGs) and targets– from poverty eradication to clean energy, gender equality to preserving biodiversity," he noted

Talking about the challenges they face in running the Vikuge farm, Farm Manager Mr Reuben Ngailo said lack of equipment and human resources hinder their plans to clean up the farm and expand production.

He stated that the farm has weeds and to uproot it costs money which brings them to running pasture production in a small field.

Scanned with CamScanner